

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Baruapepe : press@ikulu.go.tz  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

Zanzibar  
31 Agosti, 2023

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### WADAU WA MAENDELEO WASHIRIKIANE NA SERIKALI KULETA MAENDELEO - SAMIA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa Watanzania kujitokeza kutoa maoni kwa ajili ya maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050.

Rais Samia ametoa wito huo leo wakati wa hafla ya kilele cha tamasha la Kizimkazi lililofanyika katika viwanja vya Kashangae, Paje.

Aidha, Rais Samia amesema Wizara ya Mipango na Uwekezaji kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha zimeanza maandalizi ya dira hiyo ili kupata dira jumuishi yenye kukidhi mahitaji ya taifa katika kipindi cha miaka 25 ijayo.

Kwa upande mwingine, Rais Samia amesema Tamasha la Kizimkazi ni la muhimu kwa wananchi kwa kuwa husaidia kuzinduliwa kwa miradi inayofadhiliwa na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Rais Samia pia ametoa wito kwa wadau wengine wa maendeleo kushirikiana na serikali kupunguza na kuondoa changamoto zinazoendelea kujitokeza katika mkoa wa Kusini.

Vile vile, Rais Samia amesema serikali ina mpango wa kutekeleza mradi wa *Jenga Kesho iliyo Bora* visiwani Zanzibar ili kuwawezesha vijana wengi kujajiri mkoani humo.

Hali kadhalika, Rais Samia amewataka wananchi kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kufanikisha harakati za kuleta maendeleo ya uchumi kwa maslahi ya jamii na taifa kwa ujumla.

Zuhura Yunus  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

